



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26 - 2963822
Nukushi: +255 26 - 296382
Barua pepe: sg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2683
Dodoma
TANZANIA



Kumb. Na. BE. 424/448/01/43

Tarehe: 16 Agosti, 2022

TAARIFA KWA UMMA WATALII WALIOINGIA NCHINI, KIPINDI CHA JANUARI - JULAI, 2022

Taarifa ya mwenendo wa watalii walioingia nchini ni miongoni mwa taarifa za mara kwa mara (high-frequency data) zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu SURA 351.

Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Januari - Julai 2022

Idadi ya watalii kutoka nje ya nchi waliotembelea vivutio mbalimbali vya utalii katika kipindi cha Januari hadi Julai 2022 waliendelea **kuongezeka hadi 742,133** ikilinganishwa na watalii **456,266** walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2021, ikiwa ni sawa na **asilimia 62.7 (Jedwali Na. 1)**. Kati ya watalii 742,133 walioingia nchini, watalii **222,449** waliingia nchini kupitia Zanzibar ambao ni sawa na asilimia **30.0** ya watalii wote.

Watalii walioingia nchini mwezi Julai 2022 pekee, **waliongezeka hadi 166,736** ikilinganishwa na watalii **81,307** walioingia nchini mwezi Julai 2021, sawa na ongezeko la asilimia **105.1**. Idadi ya watalii walioongezeka mwezi Julai 2022 ilikuwa zaidi ya mara mbili ya watalii walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2021.

Jedwali Na. 1: Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Kuanzia Januari hadi Julai 2022

Mwezi	2021	2022	Ongezeko	Badiliko (%)
Januari	79,116	94,441	15,325	19.4
Februari	79,730	101,042	21,312	26.7
Machi	72,285	93,889	21,604	29.9
Aprili	43,966	79,405	35,439	80.6
Mei	42,173	89,271	47,098	111.7
Juni	57,689	117,349	59,660	103.4
Julai	81,307	166,736	85,429	105.1
Jumla	456,266	742,133	285,867	62.7

Chanzo: Jeshi la Uhamiaji - Agosti 2022

Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Januari hadi Julai 2022 kwa Mchanganuo wa Utaifa

Idadi kubwa ya watalii walioingia nchini kutoka nchi zilizo nje ya Bara la Afrika kwa mchanganuo wa utaifa katika kipindi cha Januari hadi Julai 2022 walitoka Marekani

ikiwa na watalii 51,301. Nchi nyingine zilikuwa Ufaransa (47,403), Ujerumani (30,817), Poland (29,004) na Uingereza (28,275). Aidha, katika mwezi Julai 2022 pekee, idadi kubwa ya watalii walioingia nchini walitoka Marekani (17,135), Ufaransa (12,634), Uingereza (8,586), Ujerumani (8,015) na Netherland (5,102).

Tanzania pia ilipokea watalii kutoka katika Bara la Afrika ambapo katika kipindi cha Januari hadi Julai idadi kubwa ya watalii walitoka Kenya (86,220), Burundi (54,877), Malawi (27,079), Uganda (21,080) na Afrika Kusini (20,868). Vilevile, katika kipindi cha mwezi Julai 2022 pekee idadi kubwa ya watalii walioingia nchini walitoka Kenya (16,654), Burundi (7,966), Malawi (5,113), Afrika Kusini (4,335) na Rwanda (4,035).

Kutokana na umuhimu wa Sekta ya Utalii katika kuingiza fedha za kigeni nchini, taasisi zinazotoa huduma kwa watalii zina wajibu wa kuendelea kuboresha zaidi huduma kwa lengo la kuendelea kuvutia watalii wapya na wanaokuja nchini kwa mara nyingine.

Kwa mujibu wa Sera ya Mapitio ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, takwimu za idadi ya watalii wanaoingia nchini zinaweza kufanyiwa mapitio endapo takwimu mpya na zilizohuishwa kutoka kwenye chanzo zitapatikana.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na Mtakwimu Mkuu wa Serikali S.L.P 2683 Dodoma, Simu +255 26 2963822, Nukushi +255 26 296382, Barua pepe: sg@nbs.go.tz, tovuti: www.nbs.go.tz



Nipo Tayari Kuhesabiwa Tarehe 23 Agosti, 2022